

Machi 10, 2026

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA JARIDA LA MTANDAONI



MFUKO

BIMA

Kujiunga

Scan Hapa



NHIF: BIMA YA AFYA KWA WOTE YAANZA NA USAJILI WA KAYA ZISIZO UWEZO

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeleza kuwa utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote umeanza kwa usajili wa kaya zisizo na uwezo. Imeelezwa kwa Mfuko kupitia mifumo iliyoboreshwa na mtandao mpana wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini upo tayari kuwahudumia wananchi.

Kauli hiyo imetolewa wakati wa kikao kazi cha viongozi waandamizi wa NHIF kilichofanyika jijini Arusha, kilichowakutanisha viongozi kutoka Makao Makuu, ofisi za mikoa pamoja na ofisi ndogo za Mfuko.

Kikao hicho kililenga kupokea na kujadili taarifa ya

maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote pamoja na kuweka mikakati ya kuimarisha utoaji wa huduma kwa wanachama.

Katika kikao hicho, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dkt. Irene Isaka, alipokea taarifa ya utekelezaji wa mpango huo kuanzia zoezi la usajili na utambuzi wa kaya maskini pamoja na ukaguzi wa utayari wa vituo vya kutolea huduma kwa wanachama wa Mfuko.

Ripoti ya uhakiki wa vituo vya kutolea huduma imeonesha kuwa vituo vingi vipo tayari kutoa huduma kwa wanachama, na tayari baadhi ya wananchi waliojiunga wameanza kunufaika kwa

Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge Sasa



www.nhif.or.tz



@nhiftz



0800 787800



NHIFOnlineTv

kupokea huduma katika vituo hivyo.

Akizungumza katika kikao hicho, Dkt. Isaka alieleza kuwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na Mfuko katika mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) umeleta mapinduzi katika utoaji wa huduma kwa wadau wa NHIF.

Alifanua kuwa katika hatua ya kuboresha huduma, Mfuko umeimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Uchakataji Madai, ambao utawawezesha watoa huduma kuwasilisha madai yao kwa wakati na kwa urahisi bila ya kutumia fomu za karatasi.

“Uwekezaji huu katika mifumo ya TEHAMA umeimarisha ufanisi na uwazi katika utoaji wa huduma. Aidha, hatua hii inaenda sambamba na juhudi za Serikali za kulinda mazingira kwa kupunguza matumizi ya karatasi katika shughuli za kila siku,” alisema Dkt. Isaka.

Kwa upande wao, viongozi wa NHIF kutoka mikoa mbalimbali walieleza utayari wao kwa utekezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

Aidha, baadhi ya viongozi walieleza kwamba zoezi hili limeweza kubaini wanufaika hewa, wanufaika ambao si maskini, wanufaika waliofariki na wanufaika waliohama. Walieleza changamoto kubwa ni athari za mvua lakini wakasisitiza kuwa changamoto hizo hazikuzuia jitihada za kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kwa mafanikio.

Mbali na kupokea taarifa ya utekezaji wa mpango huo, kikao hicho pia kilijadili mpango mkakati wa Mfuko na namna bora ya kuufikisha katika dira yake ya kuwa taasisi kinara katika utoaji wa huduma za bima ya afya nchini na Afrika kwa ujumla.

Viongozi walitoa maoni na mapendekezo mbalimbali yatakayosaidia kuboresha zaidi utekezaji wa majukumu ya Mfuko, huku wakiahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano ili kutekeleza maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na Maelekezo ya Waziri wa Afya Mh. Mchengerwa (MB) kwa NHIF kuhakika wa huduma za afya kupitia mfumo wa bima unawafikia wananchi.

HABARI PICHA



Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge Sasa



www.nhif.or.tz



@nhiftz



0800 787800



NHIFOnlineTv